**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**Juni, 2024**

**Dodoma**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0763067607,0625616288**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0758994988**
**Matron:0747085523**

**Shule ya Sekondari Mkugwa,**

**S.L.P 121,**

**Tarehe .17 April 2024**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MKUGWA HALMASHAURI YA (W) KIBONDO MKOA WA KIGOMA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **2024** na atasoma tahasusi ya ………….........

Shule ya Sekondari Mkugwa ipo willaya ya kibondo umbali wa Kilometa 40 Kaskazini Magharibi mwa Mji wa **Kibondo** Usafiri wa basi kutoka Kibondo mjini unapatikana katika kituo cha mabasi Kibondo/Kituo na kituo cha Hospital ya wilaya kibondo kwa Nauli ya Shilingi **4,000/=** kwa Gari aina zote. Kwa wale wanaotoka Mikoa ya Mwanza,Geita,Kahama, Shinyanga,Tabora unaweza kupanda gari la kwenda moja kwa moja Kasulu au Kigoma shuka Mkugwa sekondari baada ya kutoka kijiji cha kifura, kwa wanaotoka Kigoma, Kasulu panda gari moja kwa shuka shule ya sekondari Mkugwa.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **1 Julai 2024**, mwanafunzi wa kidato cha Tano anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **14 Julai 2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31 Julai 2024.**

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni Sketi Rangi ya chungwa(**orange**) mbili **urefu unaogusa kiatu** kwa ajili ya vipindi vya darasani **mshono ni linda box mbele na nyuma yenye malinda manne kushoto na kulia**

ii. Sketi mbili nyeusi **urefu unaogusa viatu**, kitambaa cha sukarisukari mashono ni **marinda mapana ya kupanga** hii ni sale ya kuvaa wakati wa shughuli za nje ya darasani(Shamba dress).



**Sketi(orange**



**Sketi Nyeusi(sukarisukari)**



**T-Sheti(Kijivu)**



**Sweta dark blue**

iii. (*ambatisha kipande cha kitambaa na picha ya mshono);*

iv. Mashati **Mawili meupe mikono** mirefu.

v. **T-shirt mbili** zenye **<u>ukosi(form six)</u>** moja rangi ya **kijivu** na nyingine rangi ya **chungwa.(unaweza ipata duka la shule kwa shilingi 13000/=) kwa kila T-shirt moja**

vi. Rangi ya Hijab (kijuba) ni Nyeupe kwa muda wa darasani na nyeusi baada ya vipindi vya darasani ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama.

vii. Sare ya Michezo ni **traki suti dark blue** isimbane mwanafunzi anapoivaa na **T-shirt Nyekundu**(form six) isiyokuwa na mapambo au maandishi yoyote.

*Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;*

viii. Soksi jozi mbili nyeupe na nyeusi za shule;

ix. Sweta moja **Dark blue. (unaweza kulipata shuleni kwa shilingi 15000/=)**

x. Tai mbili rangi ya chungwa zinapatikana duka la shule kwa shilingi 4000/-

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Wanafunzi wote wanatakiwa kuja na **Bima ya Afya ya NHIF** shuleni aidha mwanafunzi ambaye hatakuja nayo hatapokelewa shuleni

ii. Madaftari counterbook Quire 3/Quire4 kumi(**10**)

iii. **Ream (A4)** Mbili (2) za Karatasi.

iv. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.

v. Godoro kwa wanafunzi wote liwe na vipimo vya $2^1/_2$,kwa sita

vi. Mashuka jozi 2 rangi ya pink,blanket 1,foronya ya godoro 1, chandarua 1 (nyeupe)

vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe)

viii. Ndoo 2 ndogo (lita kumi) zenye mifuko

ix. Dissecting Kit kwa wanafunzi wanaosoma Biology;

x. Scientific Calculator;

xi. Nguo za ndani za kutosha pamoja na taulo.

**Orodha ya vitabu ambavyo mwanafunzi anatakiwa kuja navyo kulingana na mchepuo wake au Tahasusi yake.**

**HGL**

| Na | SOMO-ENGLISH LANGUAGE | VITABU |
|---|---|---|
| 1 | Literature- plays | Betrayal in the City- Francis Imbuga |
| | | I will Marry When i want-Ngugi wa Thiongo |
| | | An Enemy of the people-Henrik Ibsen |
| **2** | Novels and short stories | Encounters from Africa- Macmillan Education Limited. |
| | | The Beutifull one are not yet born- Ayeki Kweirmah |
| | | A Seaason of Waiting- David Omowale |
| **3** | Poetry | Selected poems- Tanzania institute of Education. |
| | | The wonderfull Surgeon and other poem by Charles Mloka. |
| **4** | **GEOGRAPHY** | Practical Geography. |
| | | Long-man Atlas & Map sheets |
| | | Physical Geography D.T Msabila. |
| | | Human and Economic Geography |
| **5** | **HISTORY** | History for Secondary School Form 5&6 Shiitali & Salehe Yassini |
| **6** | **GENERAL STUDIES** | Understanding Advanced level General studies(2016)- Joannes Bigirwamungu & Sospeter Deogratius Mikoani Publisher Dar es Salaam |

**HKL**

| Na | SOMO-ENGLISH | VITABU |
|---|---|---|
| 1 | Literature- plays | Betrayal in the City- Francis Imbuga |
| | | I will Marry When i want-Ngugi wa Thiongo |
| | | An Enemy of the people-Henrik Ibsen |
| **2** | Novels and short stories | Encounters from Africa- Macmillan Education Limited. |
| | | The Beutifull one are not yet born- Ayeki Kweirmah |
| | | A Seaason of Waiting- David Omowale |
| **3** | Poetry | Selected poems- Tanzania institute of Education. |
| | | The wonderfull Surgeon and other poem by Charles Mloka. |
| **4** | **KISWAHILI** | Kwenye Ukingo wa Thim-Ebrahim Hussein |
| | | Chungu Tamu- T.A Mvungi |

| | | |
|---|---|---|
| **5** | **HISTORY** | History for Secondary School Form 5&6 Zombwe& Zist Kamili |
| | **GENERAL STUDIES** | Understanding Advanced level General studies(2016)- Joannes Bigirwamungu & Sospeter Deogratius Mikoani Publisher Dar es Salaam |

**HGK**

| **Na** | **SOMO** | **VITABU** |
|---|---|---|
| **1** | **KISWAHILI** | Kwenye Ukingo wa Thim-Ebrahim Hussein. |
| | | Chungu Tamu-T.A Mvungi. |
| **2** | **GEOGRAPHY** | Practical Geography |
| | | Long-man Atlas, & Map sheets |
| | | Physical Geography |
| | | Human and Economic Geography |
| **3** | **HISTORY** | History for Secondary School Form 5&6 Zombwe<br>& Shibitali |
| **4** | **GENERAL STUDIES** | Understanding Advanced level General studies(2016)- Joannes Bigirwamungu & Sospeter Deogratius Mikoani Publisher Dar es Salaam |

**EGM**

| **Na** | **SOMO** | **VITABU** |
|---|---|---|
| **1** | **ECONOMICS** | Morden Economic Theory- Dr K.K Dewett & M.H Navalur |
| | | Principles of Economics Vol 7. Adam Smith. |
| **2** | **GEOGRAPHY** | Practical Geography- Shibitali |
| | | Physical Geography-D.T Msabila. |
| | | Long-man Atlas & Map sheets |
| | | Human and Economic Geography-D.T Msabila |
| **3** | **ADV-MATH'S** | Pure Mathematics 1&2 S.Chand |
| | **GENERAL STUDIES** | Understanding Advanced level General studies(2016)- Joannes Bigirwamungu & Sospeter Deogratius Mikoani Publisher Dar es Salaam |

**CBG**

| **Na** | **SOMO** | **VITABU** |
|---|---|---|
| **1** | **CHEMISTRY** | Chemistry Book XI&XII-S.Chand |
| **2** | **BIOLOGY** | Biological science(BS) |
| **3** | **GEOGRAPHY** | Practical Geography- Shibitali |
| | | Long-man Atlas & Map sheets |
| | | Physical Geography-D.T Msabila |
| | | Human and Economic Geography |
| **4** | **BASIC A.** | Basic Applied Math's for A.Level |

| | | |
|---|---|---|
| | **MATH'S(BAM)** | |
| **5** | **GENERAL STUDIES** | Understanding Advanced level General studies(2016)- Joannes Bigirwamungu & Sospeter Deogratius Mikoani Publisher Dar es Salaam |

**PCB**

| **Na** | **SOMO** | **VITABU** |
|---|---|---|
| **1** | **PHYSICS** | Physics for Advanced level 5&6 |
| **2** | **CHEMISTRY** | Chemistry Book XI&XII-S.Chand |
| **3** | **BIOLOGY** | Biological science(BS) |
| | **BASIC A. MATH'S(BAM)** | Basic Applied Math's for A.Level. |
| | **GENERAL STUDIES** | Understanding Advanced level General studies(2016)- Joannes Bigirwamungu & Sospeter Deogratius Mikoani Publisher Dar es Salaam |

**Mwanafunzi anunue vifaa vifuatavyo aje navyo anapofika shuleni kwa tahasusi kama ifuatavyo;**

**HGK**

i. Watakuja na Kwanja 1, jembe na mpini 1, reki l, mfagio wa chelewa, hard broom na soft broom

**HGL**

ii. Watakuja na kotama 1, jembe na mpini, mfagio wa chelewa na hardbroom1, soft broom 1 na reki 1

**HKL**

iii. Watakuja na Kotama, jembe na mpini ,mfagio wa chelewa, hardbroom na soft broom na reki

**PCB**

iv. Wataleta kwanja 1, jembe na mpini, mfagio wachelewa, hardbroom na softbroon

**CBG**

v. Wataleta kwanja 1, jembe na mpini, mfagio wa chelewa, hardbroom1, soft broom 1.

**EGM**

vi. Wataleta kwanja 1, jembe na mpini, mfagio wa chelewa, hardbroom 1, soft broom 1 na reki 1.

### 2.3 Michango mbalimbali

a) **Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**NB: Michango yote inatakiwa kulipwa kwenye akaunti ya shule banki ya NMB, Akaunti NO.51501000017 jina la akaunti SHULE YA SEKONDARI MKUGWA/MKUGWA SEKONDARI.**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku(Night Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;

viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;

xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

**Saini ya Mkuu wa Shule** 

**Jina la Mkuu wa Shule: Martha Myaniko Kajoro**

**Mhuri wa Mkuu wa Shule** 

**NB:** **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0763067607, 0625616288**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0758994988,0628793382**
- **Mwandamizi Taaluma :0629450158,0742809445**
- **Mwandamizi Malezi; 0753875689.**

## SHULE YA SEKONDARI MKUGWA
**S.L.P 121 KIBONDO**

FOMU NAMBA 1

## HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. Jinala mwanafunzi………………………..
2. Jina la baba………………………………..
3. Jina la mama……………………………….
4. Jina kamili la mzazi/mlezi…………………
5. Anuani ya mzazi/mlezi…………………….
6. Uhusiano wa mzazi/ mlezi………………….
7. kazi ya baba (mkulima, mfanyabiashara,mfanyakazi)…………………
8. Kama nimkulima zao muhimu analolitegemea ni…….............................
9. Kama ni mfanyabiashara, biashara anayoitegemea ni..................................
10. Kama ni mfanyakazi kazi yake ni.........................................……
11. Afya ya mwanafunzi, kama anayo matatizo ya kiafya na hivyo kustahili huduma maalum mzazi au mlezi aeleze……………………………………
12. Dhehebu/ dini anayosali mwanafunzi....……………………
13. Jamaa na ndugu wanaoruhusiwa kumtembelea mwanafunzi kwa ruhusa ya mzazi/mlezi:-

Jina kamili Kazi yake Namba ya simu

Bandika picha

a.………………………… ……………….

Bandika picha

b)....................................... ...............................

Bandika picha

c)....................................... ...............................

## SHULEYA SEKONDARI MKUGWA
**S.L.P. 121 KIBONDO**

**FOMU NAMBA 2**

# FOMU YA KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE

Jina la rnwanafunzi ...........................................................................................

Anuani ya mzazi / mlezi..............................................................................

Mimi kama Mtanzania na amini kuwa nimetunukiwa nafasi hiyo niliyopewa na umma wa Tanzania.

Hivyo naahidi kuwa nita jibidiisha kadri ya uwezo wangu wote katika kazi zote nitakazopewa hapa shuleni nje na ndani ya darasa ili kuleta ufanisi.

Ili kutimiza shabaha hiyo ninakubali na nime ahidi kwa hiari yangu rnwenyewe kuwa nitaífanya

kazi kwa BUSARA, JUHUDI YA HALI YA KABISA NA KUTII kwa viongozi wote wa shułe parnoja na sheria. Nikiwa na maoni au malałamiko ni na ahidi ni tayafikisha panapo husika kwa njia na taratíbuzinazokubalika, .

| …………………………… | ……………... | ………… |
|---|---|---|
| JINA LA MWANAFUNZI | TAREHE | SAINI |

**KIAPO CHA MZAZI KUMSOMESHA MTOTO.**

Mimi mzazi wa .......................................................................................

Ninakubali na kuahidi kuwa niko tayari kumsomesha na kumlipia ada na michango yote ya shule kwa wakati. Hivyo nitahakikisha ninashirikiana na shule kufatilia maendeleo ya taaluma

na malezi ya mwanangu kwa ukaribu. Kwa kipindi chote atakachokuwa shuleni Nitahakikisha mwanafunzi wangu anakuwa mfano bora wa kuigwa na wenzake.

| ..................................................... | ........................... | ............................. |
|---|---|---|
| JINA LA MZAZI/MLEZI | SAHIHI | TAREHE |

SHULEYA SEKONDARI MKUGWA

S.L.P 121 KIBONDO

FORM NUMBER 03

# MEDICAL EXAMINATION FORM

To medical Officer I/C OF

..........................................................................................................

Designated Hospital, PO. BOX

_______________________________________________________________

Please examine the above named in full as to his/her physical and mental fitness for being able to pursue two years of secondary school educations The examination should include categories

In case of any acute or defect/ disability in each category or sub-category, may render the aspirant ineligible of admission or eligible of admission to schools of students with special needs.

a) Pupil's name ________________________________________

c) Stool ____________________________________________

d) Blood group _______________________________________

e) Urine analysis ______________________________________

f) Sphills test_________________________________________

g) Chest test__________________________________________

h) Eye test____________________________________________

i) Sickle cell test ______________________________________

j) Abdomen test_______________________________________

k) WCB Differential _____________________________________

Additional information and physical defect or impairment to pursue further studies

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

Signed by ______________________________________________

Designation_____________________________________

Official stump_________________________________

Date___________________________________